**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# RATIBA YA SHUGHULI ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE KUANZIA TAREHE 05 HADI 25 OKTOBA, 2026

---

Idara ya Kamati za Bunge,
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 941
40490 Tambukareli,
**DODOMA**

## YALIYOMO


**1.0 UTANGULIZI ........ ii**

1.1 Maelezo ya Jumla ........ ii

1.2 Shughuli Zilizopangwa ........ ii

1.1.1 Kuchambua Sheria Ndogo ........ ii

1.1.2 Kupokea na kujadili Taarifa Mbalimbali za Utendaji wa Serikali na Taasisi zake ........ ii

1.1.3 Kuchambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2024/2025 ........ iii

1.1.4 Kupokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ........ iii

1.1.5 Kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha 2027/2028 ........ iii

**2.0 RATIBA YA KILA KAMATI YA KISEKTA ........ 1**

2.1 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ........ 1

2.2 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ........ 5

2.3 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ........ 8

2.4 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ........ 11

2.5 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ........ 14

2.6 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ........ 22

2.7 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ........ 24

2.8 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ........ 27

2.9 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ........ 32

2.10 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ........ 35

2.11 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ........ 39

**3.0 RATIBA YA KILA KAMATI YA SEKTA MTAMBUKA ........ 42**

3.1 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ........ 42

3.2 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) ........ 45

3.3 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ........ 45

**4.0 RATIBA YA KILA KAMATI INAYOSIMAMIA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA ........ 50**

4.1 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ........ 50

4.2 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ........ 55

**RATIBA YA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE KUANZIA TAREHE 05 HADI 25 OKTOBA, 2026**

---

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Maelezo ya Jumla

Mkutano wa Tano wa Bunge utaanza siku ya Jumanne, tarehe 27 Oktoba, 2026. Kama ilivyo ada, Mkutano huo utatanguliwa na Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge kumi na sita (16), ambapo Kamati tano (05) zitatangulia kuanza vikao tarehe 05 Oktoba, 2026 na Kamati kumi na moja (11) zitaanza vikao tarehe 12 Oktoba, 2026. Kamati zitakazotangulia ni:

(i) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo;
(ii) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC);
(iii) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC);
(iv) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC); na
(v) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Kamati hizo hutangulia kutokana na utaratibu wa Bunge kutekeleza wajibu wake wa kufuatilia utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokabidhiwa serikalini, mahitaji ya Kamati kuhusu muda wa uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, utekelezaji wa jukumu la Bunge kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma (Public Investment) kupitia Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) na majadiliano ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha 2027/2028 kupitia Kamati ya Bajeti.

Kamati kumi na moja (11) zilizosalia zitaanza vikao tarehe 12 Oktoba, 2026. Vikao vya Kamati zote kumi na sita (16) vitakamilika ifikapo tarehe 25 Oktoba, 2026.

## 1.2 Shughuli Zilizopangwa

Shughuli za Kamati katika kipindi hicho zinajumuisha maandalizi ya shughuli za Mkutano wa Nne wa Bunge na shughuli nyingine za ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za umma kama ifuatavyo: -

### 1.1.1 Kuchambua Sheria Ndogo

Sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nne wa Bunge zitachambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Shughuli hiyo imepangwa kufanyika kwa mujibu wa fasili ya 10(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

### 1.1.2 Kupokea na Kujadili Taarifa Mbalimbali za Utendaji wa Serikali na Taasisi zake

Kamati kumi na moja za kisekta zitapokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Serikali na Taasisi zake. Shughuli hii imepangwa kwa mujibu wa fasili ya 7(c) na (d) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Aidha, Kamati ya Bajeti itapokea na kujadili taarifa mbalimbali kutoka Serikalini

kwa lengo la kutekeleza jukumu lake la kusimamia, kuchambua, kuratibu na kulishauri Bunge kuhusu sera za fedha za umma, mapato ya Serikali, Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

### 1.1.3 Kuchambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2024/2025

Kamati mbili za kusimamia Matumizi ya Fedha za Umma zitachambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu hesabu zilizokaguliwa za wizara, taasisi, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2025. Shughuli hii imepangwa ili kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kwa mujibu wa fasili ya 13, fasili ya 14 na fasili ya 15 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kamati zinazohusika ni Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

### 1.1.4 Kupokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) itapokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na miongozo mujarabu ya biashara. Shughuli hii itafanyika kwa mujibu wa fasili ya 11(1) na (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

### 1.1.5 Kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha 2027/2028

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti itapokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Mwaka wa Fedha 2027/2028 ili kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kuhusu Mwongozo wa kuandaa Bajeti ya Serikali, vyanzo vya mapato ya Serikali na Mapendekezo ya Mpango wa Serikali na vipaumbele kuhusu Mpango huo. Shughuli hii itafanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 116(1) - (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

**2.0 RATIBA YA KILA KAMATI YA KISEKTA**

**2.1 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria**

**Ukumbi**: Frank Mfundo - Ghorofa ya 5, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>11 Oktoba, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>12 Oktoba, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala;<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026;<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (SBUU) kuhusu -<br>(i) hatua zilizochukuliwa katika kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa sera, mipango na miradi ya Serikali, pamoja na matokeo yaliyopatikana katika ufuatiliaji huo; na<br>(ii) hatua zilizochukuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa katika kuimarisha usimamizi na udhibiti wa shughuli za vyama vya siasa kwa kuzingatia Sheria, ikiwemo kuhakikisha uzingatiaji wa matakwa ya kisheria, uwazi na uwajibikaji katika uendeshaji wa vyama vya siasa nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti<br>☞ WN-OWM (SBUU) |
| **Jumanne**<br>13 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (SBUU) kuhusu -<br>(i) hatua za tahadhari na maandalizi zinazochukuliwa na Serikali kukabiliana na athari zinazoweza kusababishwa na mvua za El Niño nchini, hususani katika maeneo yenye uwezekano mkubwa wa kukumbwa na maafa ya mvua hizo; na<br>(ii) taarifa ya utekelezaji kuhusu Mfumo Shirikishi wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji (NEMIS), ikiwemo kiwango cha matumizi yake katika kufuatilia programu za uwezeshaji, wanufaika na matokeo ya utekelezaji wa shughuli hizo: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (SBUU) |
| **Jumatano**<br>14 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE** | **WOTE** |
| **Alhamisi**<br>15 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais (MUUUB) kuhusu hatua zilizochukuliwa na Watumishi Housing Investments (WHI) katika kuongeza upatikanaji wa nyumba za gharama nafuu kwa watumishi, ikiwemo | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR-MUUUB |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| | utekelezaji wa miradi ya makazi, idadi ya nyumba zilizokamilika na zinazotarajiwa kujengwa, pamoja na hatua za kuwezesha watumishi kumiliki nyumba kwa njia nafuu na zinazozingatia uwezo wao kifedha. | |
| **Ijumaa**<br>16 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais (MUUUB) kuhusu -<br>(i) hatua zilizofikiwa katika zoezi la kuhamisha umiliki wa ndege zilizokodishwa kwa ATCL kutoka TGFA kwenda ATCL, pamoja na kukamilisha uchambuzi wa taarifa muhimu zinazohitajika kwa ajili ya kuingia mikataba ya uhamisho wa ndege hizo; na<br>(ii) hatua zilizofikiwa katika taratibu za ununuzi wa ndege mpya kwa ajili ya TGFA, ikiwemo aina ya ndege zinazotarajiwa kununuliwa, hatua zilizochukuliwa hadi sasa, pamoja na mipango ya matengenezo ya ndege zilizopo. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR-MUUUB |
| **J'mosi & J'pili**<br>17 & 18 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>19 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais (MU) kuhusu -<br>(i) hatua zilizochukuliwa katika kuratibu na kurahisisha mifumo ya ulipaji kodi na utoaji wa leseni za biashara, ikiwemo kuanzisha mfumo mmoja wa utoaji leseni na kuweka taarifa za leseni zinazohitajika kwa sekta mbalimbali za uwekezaji kupitia tovuti ya TISEZA; na<br>(ii) hatua zilizochukuliwa katika kuimarisha ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya uwekezaji, hususan miradi yenye kuchelewa au kutofikia malengo yaliyowekwa, pamoja na hatua za kukabiliana na changamoto zinazoathiri utekelezaji wake. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR-MU |
| **Jumanne**<br>20 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu -<br>(i) hatua zinazochukuliwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika na upelelezi, ukamataji na utaifishaji wa mali katika kuhakikisha haki za watuhumiwa zinalindwa na mali zao zinatunzwa ipasavyo bila kupoteza thamani hadi mashauri yanayowahusu yapohitimishwa mahakamani; na | ☞ Wajumbe<br>☞ WKS |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| | (ii) hatua zilizochukuliwa katika kupitia na kufanya marekebisho ya Sheria 41 zilizobainika kukinzana, ikiwemo kifungu cha 80(2) cha Sheria ya Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi, Sura ya 263, ili kuondoa mkanganyiko wa kisheria na changamoto za tafsiri katika utekelezaji wa Sheria hizo. | |
| **Jumatano**<br>21 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais (MM) kuhusu -<br>(i) hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuharakisha ujenzi wa ofisi na majengo ya kudumu kwa Taasisi za Muungano upande wa Zanzibar; na<br>(ii) ushirikiano uliopo kati ya Tanzania Zanzibar na Tanzania Bara katika sekta ya gesi na mafuta, usajili wa magari na sekta ya afya katika kuimarisha Muungano: Mafaniko, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OMR-MM |
| **Alhamisi**<br>22 Oktoba, 2026 | ☞ Kufanya Majadiliano ya Pamoja kuhusu Miaka Mitano ya Kituo Jumuishi cha Mahakama cha Masuala ya Familia na Mirathi – Temeke: Mchango katika ustawi wa familia na maendeleo ya Taifa. | ☞ Wajumbe<br>☞ WKS<br>☞ MMM<br>☞ WMJWM<br>☞ Kituo Jumuishi Mahakama Temeke |
| | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu -<br>(i) hatua zilizochukuliwa na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (LST) katika kutekeleza mfumo wa LST e-FIELD MIS 2026 na mtaala wa *Practice-Based Practical Learning*: Kiwango cha matumizi ya mfumo, changamoto na matokeo yaliyopatikana katika kuboresha mafunzo ya vitendo na kuwaandaa wanafunzi kukidhi mahitaji ya soko la ajira; na<br>(ii) hatua zilizochukuliwa na RITA katika kuboresha na kuimarisha huduma za usajili na uhifadhi wa kumbukumbu za matukio ya kijamii nchini kupitia mfumo wa eRITA, katika kuongeza ufanisi, kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi, kuimarisha uhakika na usalama wa | ☞ Wajumbe<br>☞ WKS |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
| --- | --- | --- |
| | taarifa, pamoja na kudhibiti matumizi ya nyaraka zisizo halali. | |
| **Ijumaa**<br>23 Oktoba, 2026 | ☞ Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>24 & 25 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WN-OWM (SBUU)** - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu)
- ☞ **WN-OR-MUUUB** - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora
- ☞ **WN-OR-MU** - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Mipango na Uwekezaji
- ☞ **MMM** - Mtendaji Mkuu wa Mahakama
- ☞ **WKS** - Waziri wa Katiba na Sheria
- ☞ **AG** - Mwanasheria Mkuu wa Serikali
- ☞ **WMJWM** - Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu
- ☞ **WN-OMR-MM** - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- ☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz
- ☞

### 2.2 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo

**Ukumbi:** Msekwa D, Jengo la Pius Msekwa

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>11 Oktoba, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>12 Oktoba, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala;<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>13 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu utendaji wa -<br>(i) Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(ii) Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CARMATEC): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WVB |
| **Jumatano**<br>14 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE** | **WOTE** |
| **Alhamisi**<br>15 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu utendaji wa -<br>(i) Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI) na maoni ya namna ya kukuza Sekta ya Viwanda na Biashara: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(ii) Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (SIDO): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WVB |
| **Ijumaa**<br>16 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea maelezo ya Sekretarieti ya uchambuzi wa kisheria kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 (*International Sugar Agreement of 1992)*; na<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Kilimo kuhusu utendaji wa -<br>(i) Bodi ya Kahawa Tanzania: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) Bodi ya Mkonge Tanzania: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumamosi**<br>17 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea maelezo ya Waziri wa Kilimo kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 (*International Sugar Agreement of 1992);* na<br>☞ Kusikiliza na kupokea maoni ya wadau kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 (*International Sugar Agreement of 1992)*. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |
| **Jumapili**<br>18 Oktoba, 2026 | ☞ Kuchambua maoni yaliyokusanywa kutoka kwa Wadau na majumuisho ya hoja zote zilizojitokeza ili kupata jedwali la uchambuzi na hoja zinazohitaji ufafanuzi wa Serikali na kuwasilisha Serikalini jedwali la hoja zitokanazo na uchambuzi na majumuisho; na<br>☞ Kukabidhi Serikalini jedwali la hoja zitokanazo na uchambuzi kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 (*International Sugar Agreement of 1992)*. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |
| **Jumatatu**<br>19 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Kilimo kuhusu -<br>(i) utendaji wa Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) utekelezaji wa Programu ya Jenga Kesho Bora (BBT): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |
| **Jumanne**<br>20 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Kilimo kuhusu utendaji wa -<br>(i) Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI); Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) Mfuko wa Udhamini wa Pembejeo za Kilimo (AGITF): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |
| **Jumatano**<br>21 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu -<br>(i) utendaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) utekelezaji wa Programu ya Kuwezesha Vijana Kiuchumi (BBT- Mifugo na Uvuvi): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMUV |
| **Alhamisi**<br>22 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu utendaji wa -<br>(i) Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (LITA): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMUV |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Ijumaa**<br>23 Oktoba, 2026 | ☞ Kupitia rasimu ya taarifa ya maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Marekebisho ya Mkataba wa Kimataifa wa Sukari wa Mwaka 1992 (*International Sugar Agreement of 1992);* na<br>☞ Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>24 & 25 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

☞ **WVB** - Waziri wa Viwanda na Biashara

☞ **WMUV** - Waziri wa Mifugo na Uvuvi

**TANBIHI:**

☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;

☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na

☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

## 2.3 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama

**Ukumbi:** Herman Serwat - Ghorofa ya 5, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>11 Oktoba, 2026 | Wabunge kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>12 Oktoba, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>13 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais (MUUUB) kuhusu hali ya ulinzi na usalama nchini pamoja na hali ya utakatishaji fedha na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR-MUUUB |
| **Jumatano**<br>14 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE** | **WOTE** |
| **Alhamisi**<br>15 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu namna Wizara inavyoshirikiana na Wabunge wawakilishi wa Tanzania katika jumuiya mbalimbali pamoja na vyama vya kibunge katika kubeba ajenda za nchi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WNJE |
| | ☞ Kupokea na kujadili taarifa za wawakilishi wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (East Africa Legislative Assembly - EALA). | ☞ Wajumbe<br>☞ Wawakilishi wa EALA |
| **Ijumaa**<br>16 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa ujenzi wa kituo kipya cha kisasa cha Mikutano cha Mount Kilimanjaro international Convention Centre (MK - ICC). | ☞ Wajumbe<br>☞ WNJE<br>☞ Mfadhili wa mradi<br>☞ Mwakilishi wa Mkandarasi<br>☞ Mwakilishi wa Mshauri Elekezi |
| **J'mosi & J'pili**<br>17 & 18 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>19 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi kuhusu -<br>(i) hali ya usalama wa raia na mali zao nchini katika kipindi cha Julai hadi Septemba, 2026; na<br>(ii) utekelezaji wa majukumu ya Shirika la Uzalishaji Mali Magereza (SHIMA): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMNN |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumanne**<br>20 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu utendaji wa -<br>(i) Mfumo mpya wa kielektroniki wa kusimamia ukaguzi wa magari (Moter Vehicle Inspection Management Information System - MIMIS): Mafanikio, changamoto za utaratibu, na hatua za utatuzi; na<br>(ii) Chuo cha Uhamiaji cha Raphael Kubaga, Tanga: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMNN |
| **Jumatano**<br>21 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu utendaji wa -<br>(i) Chuo cha Zimamoto na Uokoaji cha Chogo, Tanga: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) Kituo cha Uchakataji wa Taarifa cha Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Kibaha, Pwani: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMNN |
| **Alhamisi**<br>22 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu -<br>(i) utatuzi wa changamoto zinazowakabili Wazee Walemavu walioshiriki kupigana Vita ya Kagera;<br>(ii) utendaji wa Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi (*Tanzania Military Academy* - TMA), Arusha: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) mafunzo ya JKT kwa vijana wa kujitolea na kwa mujibu wa Sheria: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Ulinzi na JKT |
| **Ijumaa**<br>23 Oktoba, 2026 | ☞ Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J’mosi & J’pili**<br>24 & 25 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WMNN** - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi
- ☞ **WNJE** - Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki
- ☞ **JKT** - Jeshi la Kujenga Taifa

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na

☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

### 2.4 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**Ukumbi:** Anne Makinda - Ghorofa ya Tano, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>11 Oktoba, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>12 Oktoba, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>13 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu utendaji wa -<br>(i) Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba, 2026: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(ii) Tume ya Utumishi wa Walimu katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba, 2026: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) Chuo cha Serikali za Mitaa katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Septemba, 2026: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Jumatano**<br>14 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE** | **WOTE** |
| **Alhamisi**<br>15 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) tathmini ya hali ya uchakavu wa miundombinu ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za zamani nchini na mkakati wa kuzifanyia ukarabati;<br>(ii) mkakati wa kuimarisha usafi wa mazingira kwenye halmashauri nchini; na<br>(iii) hali ya usafi wa mazingira na mkakati wa kuimarisha usafi huo katika halmashauri za -<br>a) Mkoa wa Mbeya;<br>b) Mkoa wa Dodoma; na<br>c) Mkoa wa Mwanza. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Ijumaa**<br>16 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) tathmini ya hali ya uchakavu wa shule za zamani za sekondari na msingi nchini;<br>(ii) mpango wa kuzifanyia ukarabati shule chakavu za sekondari na msingi nchini; na<br>(iii) tathmini ya utekelezaji wa programu ya ujenzi na uendeshaji wa shule za amali nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **J'mosi & J'pili**<br>17 & 18 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>19 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) tathmini ya utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Utoaji na Usimamizi wa Mikopo ya Asilimia 10 kwa akina mama, vijana na watu wenye ulemavu nchini; na<br>(ii) tathmini ya utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024 katika halmashauri nchini kwa kuzingatia sheria na kanuni za utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Jumanne**<br>20 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) tathmini ya utendaji wa masoko nchini;<br>(ii) tathmini ya utendaji wa Masoko ya Kingalu - Morogoro, Mwanjelwa - Mbeya, Nyamagana - Mwanza;<br>(iii) mahitaji ya masoko bora nchini na mkakati wa kujenga masoko bora katika halmashauri zisizo na masoko bora; na<br>(iv) mkakati wa kuwaondoa wafanyabiashara wanaofanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi katika miji, manispaa na majiji. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Jumatano**<br>21 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa Programu ya Kuboresha Kada ya Ualimu Nchini - (GPE-TSP); na<br>(ii) utekelezaji wa Mradi wa Bonde la Mto Msimbazi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Alhamisi**<br>22 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) tathmini ya upatikanaji wa huduma za maji katika hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini; na<br>(ii) mkakati wa kuimarisha upatikananji wa huduma za maji katika hospitali, vituo vya afya na zahanati nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Ijumaa**<br>23 Oktoba, 2026 | ☞ Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili** | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
| --- | --- | --- |
| 24 & 25 Oktoba, 2026 | | |

**VIFUPISHO:**

- **WN-OWM (TAMISEMI)** - Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
- **GPE-TSP** - Global Partnership for Education Teacher Support Program

**TANBIHI:**

- Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

### 2.5 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

**Ukumbi:** Mathias Kihaule - Ghorofa ya Tano, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>11 Oktoba, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>12 Oktoba, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala;<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026; na<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (KAM) kuhusu -<br>(i) mwenendo wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) katika uandikishaji wa wanachama na ukusanyaji wa michango: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) mwitikio na ufanisi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) katika utekelezaji wa hifadhi skimu kwa wanachama wa sekta isiyo rasmi: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (KAM)<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>13 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (KAM) kuhusu -<br>(i) mwenendo wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) katika kufuatilia michango ya watumishi wa umma: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) hali ya utoaji wa mafao kwa wanachama, ikijumuisha mwenendo wa kushughulikia madai na muda wa ulipaji wa mafao: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (KAM) |
| **Jumatano**<br>14 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE** | **WOTE** |
| **Alhamisi**<br>15 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (KAM) kuhusu -<br>(i) mwenendo wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) katika usajili, usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kazi, ikijumuisha idadi ya migogoro iliyopokelewa, iliyotatuliwa na inayoendelea; na<br>(ii) hali ya utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa na Tume, pamoja na hatua zinazochukuliwa | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (KAM) |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| | kupunguza mlundikano wa mashauri na kuimarisha ufanisi wa huduma. | |
| **Ijumaa**<br>16 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (KAM) kuhusu -<br><br>(i) mwenendo wa uratibu wa mashirikisho na vyama vya wafanyakazi katika kulinda haki na maslahi ya wafanyakazi; na<br>(ii) hatua zinazochukuliwa katika kushughulikia changamoto zinazojitokeza katika mahusiano kati ya Serikali, waajiri na wafanyakazi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (KAM) |
| **J'mosi & J'pili**<br>17 & 18 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>19 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kuhusu -<br><br>(i) utekelezaji wa miongozo na taratibu za uratibu wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, ikijumuisha ushiriki wa wananchi na wadau katika shughuli za Mwenge; na<br>(ii) nafasi ya mbio za Mwenge wa Uhuru katika kuhamasisha uzalendo, umoja na mshikamano wa Taifa. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR (MV) |
| **Jumanne**<br>20 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kuhusu hatua iliyofikiwa katika uundaji na uanzishaji wa mfumo wa kidijitali wa Vijana Portal (YES) ikijumuisha -<br><br>(i) huduma zinazotarajiwa kutolewa na namna mfumo huo utakavyowaunganisha vijana na fursa za maendeleo; na<br>(ii) tija inayokusudiwa baada ya kukamilika kwa mfumo, pamoja na mikakati ya kuhakikisha mfumo unatumika kwa ufanisi na kuwafikia vijana wengi zaidi. Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR (MV) |
| **Jumatano**<br>21 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuhusu utekelezaji wa mkakati wa kuzuia na kukabiliana na ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMJWM |
| **Alhamisi**<br>22 Oktoba, 2026 | ☞ Kufanya Majadiliano ya Pamoja kuhusu Miaka Mitano ya Kituo Jumuishi cha Mahakama cha Masuala ya | ☞ Wajumbe<br>☞ WKS |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| | Familia na Mirathi – Temeke : Mchango katika ustawi wa familia na maendeleo ya Taifa. | ☞ MMM<br>☞ WMJWM<br>☞ Kituo Jumuishi Mahakama Temeke |
| | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Taasisi za Ustawi na Maendeleo ya Jamii ikijumuisha hali ya utoaji wa huduma za Ustawi na Maendeleo ya Jamii kwa wananchi, tathmini ya upatikanaji wa huduma hizo na hatua zinazochukuliwa kuimarisha uwezo wa Taasisi kutoa huduma hizo. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMJWM |
| **Ijumaa**<br>23 Oktoba, 2026 | ☞ Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>24 & 25 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WN** - Waziri wa Nchi
- ☞ **OWM** - Ofisi ya Waziri Mkuu
- ☞ **KAM** - Kazi, Ajira na Mahusiano
- ☞ **MV** - Maendeleo ya Vijana
- ☞ **WMJWM** - Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu
- ☞ **WKS** - Waziri wa Katiba na Sheria
- ☞ **MMM** - Mtendaji Mkuu wa Mahakama

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- ☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz.

### 2.6 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira

**Ukumbi:** Philip Marmo - Ghorofa ya Tano, Jengo Kuu la Utawala

| TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>11 Oktoba, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>12 Oktoba, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>13 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais (MM) kuhusu -<br><br>(i) Mpango Mkakati wa kukabiliana na athari za mvua za El nino zinazotarajiwa kunyesha kwa kiwango cha juu kwenye baadhi ya mikoa nchini; na<br>(ii) uharibifu wa mazingira na utekelezaji wa zoezi la urejelezaji wa taka ngumu kwa Mkoa wa Dar es Salaam, Arusha, Morogoro, Mwanza na Mbeya. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OMR-MM |
| **Jumatano**<br>14 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE** | **WOTE** |
| **Alhamisi**<br>15 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili maombi ya BOPOA- Lake Zone kuhusu umuhimu wa kufanya mapitio ya Kifungu cha 57 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura, 291 na Kanuni zake ili kuruhusu matumizi maalumu ya Ukanda wa Mita 60 kwa shughuli za Kibandari kama ilivyoelekezwa na Tangazo la Serikali (GN) Namba 293 la Mwaka 2022 kutoka kwa taasisi zifuatazo: -<br><br>(i) Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC);<br>(ii) Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA);<br>(iii) Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na<br>(iv) Chama cha BOPOA-Lake Zone | ☞ Wajumbe<br>☞ WUC<br>☞ WN-OMR-MM |
| **Ijumaa**<br>16 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais (MM) kuhusu utekelezaji wa maazimio ya mkutano wa 12 (COP12) wa nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi wa Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OMR-MM |

| TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **J'mosi & J'pili**<br>17 & 18 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>19 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu -<br>(i) utendaji wa bodi za maji za Mabonde katika usimamizi wa vyanzo vya maji kwa mwaka 2024 hadi 2026; na<br>(ii) Mkakati wa ushirikishaji wa wadau katika uhifadhi wa vyanzo vya Maji. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Maji |
| **Jumanne**<br>20 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu thamani ya miundombinu ya maji katika Mtandao wa Maji *(Water Network)* kwa Mikoa ya Dodoma, Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro na Arusha. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Maji |
| **Jumatano**<br>21 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa miradi ya hewa ukaa kupitia miradi mbalimbali ya maji taka nchini: Mipango, mafanikio na changamoto; na<br>(ii) Mpango wa kuimarisha utoaji wa habari na mawasiliano kwa umma. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Maji |
| **Alhamisi**<br>22 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa miradi katika Mamlaka za maji kwenye miji ya Arusha, Mbeya, Morogoro na Tanga: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi.<br>(ii) utekelezaji wa mradi wa maji katika miji 28 nchini: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Maji |
| **Ijumaa**<br>23 Oktoba, 2026 | ☞ Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>24 & 25 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

☞ **WN-OMR-MM** - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira

**TANBIHI:**

☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;

☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na

☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz.

### 2.7 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo

**Ukumbi**: Namba. 49, Jengo Dogo la Utawala (Utawala Annex)

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>11 Oktoba, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>12 Oktoba, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>13 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu mikakati ya -<br>(i) ukamilishaji wa ujenzi wa vyuo vya VETA 64 vya Wilaya na Chuo 1 cha VETA cha Mkoa wa Songwe;<br>(ii) kuandikisha, kudhibiti utoro, kuacha shule na kukamilisha elimu; na<br>(iii) kuimarisha elimu jumuishi na wanafunzi wenye mahitaji maalum. | ☞ Wajumbe<br>☞ WEST |
| **Jumatano**<br>14 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE** | **WOTE** |
| **Alhamisi**<br>15 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu -<br>(i) mkakati wa kudhibiti na kuendeleza matumizi salama ya sayansi na teknolojia ya nyuklia: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(ii) mkakati wa kuimarisha na kusimamia ubora wa elimu ya juu inayotolewa na vyuo vikuu nchini; na<br>(iii) maendeleo ya utekelezaji wa mpango wa ushirikiano kati ya Taasisi za Elimu ya Juu (Vyuo) na soko la ajira (viwanda na taasisi mbalimbali). | ☞ Wajumbe<br>☞ WEST |
| **Ijumaa**<br>16 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu mikakati ya -<br>(i) utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa;<br>(ii) upatikanaji, mgawanyo na tija ya walimu katika elimu ya msingi *(basic education)*;<br>(iii) kuboresha elimu na matokeo ya ujifunzaji katika elimu ya awali, msingi na sekondari; na<br>(iv) matumizi ya TEHAMA, elimu mtandao na akili unde katika elimu ya msingi *(basic education)*. | ☞ Wajumbe<br>☞ WEST |
| **J'mosi & J'pili**<br>17 & 18 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO WA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumatatu**<br>19 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu -<br>(i) maandalizi ya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027) na maendeleo ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vitakavyotumika;<br>(ii) maendeleo ya ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu wa Dodoma; na<br>(iii) maendeleo ya ujenzi wa eneo changamani la kupumzikia wananchi katika mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma. | ☞ Wajumbe<br>☞ WHUSM |
| **Jumanne**<br>20 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu mikakati ya -<br>(i) kukuza michezo ya riadha, masumbwi, mpira wa pete na mpira wa kikapu;<br>(ii) kuimarisha usimamizi na udhibiti wa matumizi ya rasilimali fedha katika vilabu vya mpira wa miguu;<br>(iii) usimamizi na ufuatiliaji wa mifumo ya uendeshaji wa vilabu vya soka nchini; na<br>(iv) kukuza, kulinda na kutetea maslahi ya wasanii pamoja na kudhibiti uharamia wa kazi za sanaa. | ☞ Wajumbe<br>☞ WHUSM |
| **Jumatano**<br>21 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu mikakati ya -<br>(i) ujenzi wa Kituo cha Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika - Kongwa;<br>(ii) kukuza, kuhifadhi na kuendeleza mila na desturi za kitanzania: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) kuongeza masoko ya sanaa za Tanzania ndani na nje ya nchi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WHUSM |
| **Alhamisi**<br>22 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu -<br>(i) mustakabali wa ubia kati ya TBC na Kampuni ya Startimes;<br>(ii) hali ya usikivu wa TBC maeneo ya mipakani: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) hali ya Mfuko wa Maendeleo ya Michezo: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WHUSM |
| **Ijumaa**<br>23 Oktoba, 2026 | ☞ Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **J’mosi & J’pili**<br>24 & 25 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- **WEST** - Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia
- **WHUSM** - Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

**TANBIHI:**

- Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

## 2.8 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii

**Ukumbi:** Namba. 44, Jengo Dogo la Utawala (Utawala Annex)

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>11 Oktoba, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>12 Oktoba, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>13 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii -<br>(i) utendaji wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na<br>(ii) Mfuko wa uhifadhi wa wanyamapori Tanzania (TWPF). | ☞ Wajumbe<br>☞ WMU |
| **Jumatano**<br>14 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE** | **WOTE** |
| **Alhamisi**<br>15 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu utendaji wa Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA). | ☞ Wajumbe<br>☞ WMU |
| **Ijumaa**<br>16 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu utendaji wa Chuo cha Utalii Tanzania (NCT): na<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Matumizi ya Tozo ya Maendeleo ya Utalii *(Tourism Development Levy - TDL)*: Taasisi zilizopokea fedha hizo na kilichofanyika kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMU |
| **J'mosi & J'pili**<br>17 & 18 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>19 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu Utendaji wa Shirika la Nyumba Tanzania (NHC). | ☞ Wajumbe<br>☞ WANMM |
| **Jumanne**<br>20 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu Utendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (NLUPC). | ☞ Wajumbe<br>☞ WANMM |
| **Jumatano**<br>21 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu hali ya Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ WANMM |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Alhamisi**<br>22 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ardhi kuhusu -<br>(i) utendaji wa Bodi ya Usajili wa Wathamini (VRB); na<br>(ii) utendaji wa Bodi ya Usajili wa Wataalam wa Mipangomiji (TPRB). | ☞ Wajumbe<br>☞ WANMM |
| **Ijumaa**<br>23 Oktoba, 2026 | ☞ Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>24 & 25 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WANMM** - Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
- ☞ **WMU** - Waziri wa Maliasili na Utalii

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- ☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

### 2.9 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI

**Ukumbi:** Namba. 09, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>11 Oktoba, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>12 Oktoba, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 12 hadi 25 Oktoba, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>13 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu mkakati wa uzalishaji wa dawa na vifaa tiba nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Afya |
| **Jumatano**<br>14 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE** | **WOTE** |
| **Alhamisi**<br>15 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu mkakati na mpango wa kuimarisha lishe nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Afya |
| **Ijumaa**<br>16 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Magonjwa yasiyo ya kuambukiza *(Non-Communicable Diseases)*; na<br>(ii) mikakati ya kuboresha huduma za kinga. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Afya |
| **J'mosi & J'pili**<br>17 & 18 Oktoba, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>19 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu -<br>(i) hali na athari za changamoto ya afya ya akili nchini; na<br>(ii) mikakati ya kukabiliana na changamoto ya afya ya akili nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Afya |
| **Jumanne**<br>20 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Afya kuhusu utekelezaji wa majukumu ya -<br>(i) Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT);<br>(ii) Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC); na<br>(iii) Baraza la Wataalam wa Maabara Tanzania (HPRS) | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Afya |
| **Jumatano**<br>21 Oktoba, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (SBUU) kuhusu utekelezaji wa - | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
